

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA
MTIHANI WA KUHITIMU KIDATO CHA SITA**

121/2

KISWAHILI 2

(Kwa watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shulen)

Muda: Saa 3

Mwaka: 2024

Maelekezo

1. Karatasi hii ina sehemu A na B zenyе jumla ya maswali **nane (8)**.
 2. Jibu maswali yote katika sehemu A na maswali **matatu (3)** kutoka sehemu B. Swalii la **sita (6)** ni la lazima.
 3. Zingatia maagizo ya **kila sehemu** na ya **kila swalii**.
 4. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenyе wino wa **bluu** au **mweusi**.
 5. Vifaa vya mawasiliano na vitu vyote visivyoruhusiwa **havitakiwi** katika chumba cha mtihani.
 6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.



SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Wasanii huongozwa na mbinu mbalimbali katika kutunga kazi za fasihi simulizi. Onesha mbinu nne zinazotumiwa na wasanii katika kutunga igizo kisha tunga igizo fupi linalohusu "Madhara ya ukeketaji."
2. Kwa kutumia mifano, eleza dhana za kifasihi zifuatazo:
 - (a) Visasili
 - (b) Kituo bahari
 - (c) Maghani
 - (d) Muwala
 - (e) Mkarara.
3. Kwa kutoa hoja tano, fafanua umuhimu wa nyimbo katika hadithi za fasihi simulizi.
4. Soma matini ifuatayo, kisha bainisha vipengele kumi vya lugha vilivyotumika.

Napenda mahala hapa kwa heba na utukufu wake, amani, ukimya, mkolezo wa ajabu na maumbile yake. Niko kwenye ufuko, nimekaa na gazeti langu li wazi. Sisikii, sioni, ingawa ninatarajia kwa apitaye mbali atadhani kuwa nimezama kwenye habari zilizokuwa kwenye gazeti; kumbe la hasha! Nilivutiwa na uzuri wa mandhari niliyoikabili kwenye mtiririko wa watoto warukao, wapigao mbio na kufukuzana kwenye pepo zipitazo, ziingiazo na zitokazo, kwenye bahari shwari isiyo na shari.

Vindege vionekanavyo vidogo vidogo, vijisamaki vidogo vidogo mashua na ngalawa ziyoyomazo, mbele zilizotia nanga na upopo mwanana unaotekenyia hisia za mwili kwenye mazingira timamu kabisa, zilinipa raha ya dunia. Nikapigwa butwaa! Nikaachama. Nikalia huku nimetabasamu. Nikalowa machozi ya furaha. Nikasema "Asiye na mwana aelete jiwe." Nikapuliza uluzi, nikasawazika.

Kukaa hapa penye ufuko na kutembeza jicho langu kama dira huku nchi kavu na pale baharini kulinipa tajiriba si utani! Upeo wa macho, kule ambako mbingu ilioneckana imeshikana na bahari. Mbingu ni bakuli lililofunika shani kubwa ya bahari.

Jua lilikuwa likizama. Na hapo ndipo utukufu wa mandhari haya unatimilika. Mtapanyiko wa rangi mbalimbali, zilizokaliana mchafukoge, zenye kutiwa nakshi na mvuto wa ajabu, nyekundu kwa athari, manjano inayochungulia kijivu, inayoshangilia bluu, imetamakani zambarau, imedokeza nyufa nyembamba za mistari ya fedha inayokoleza. Hakika mkono huu unajua kuchora. Nikajisemea moyoni Maulana! Jalali! Rabana!

Sarifu rangi zote unavyopenda. Sema milima na mabonde ya peponi ndivyo; sema konde ya mafuta na makorongo sawa; sarifu vingine, tazama sasa yule mpiganaji, naye pia ana upanga wake yuko juu ya farasi ikiakisi picha hii kwa jicho lake, ifuate; utaiona imekamilika sura hii hii haina hatima ya tafsiri, ndio maana waandishi na wachoraji wameandika na kuchora usanifu wa mwanadamu au maneno yaliyochorwa kwa ufasaha yanashindwa kukamilisha athari ya kuchwa kwa jua lile na athari ya mnaso wa sumaku; kwa wanaojua kutafsiri kwao wote ni miujiza.

SEHEMU B (Alama 60)

Jibu maswali **matatu** (3) kutoka sehemu hii. Swali la **sita** (6) ni la lazima.

ORODHA YA VITABU

USHAIRI

Kimbunga	-	Haji Gora
Mapenzi Bora	-	Shabani Robert
Chungu Tamu	-	Theobald A. Mvungi
Fungate ya Uhuru	-	Mohamed S. Khatibu.

RIWAYA

Usiku utakapokwisha	-	Mbunda Msokile
Kufikirika	-	Shabani Robert
Mfadhibi	-	Hussein Tuwa
Vuta N'kuvute	-	Shafi Adam Shafi

TAMTHILIYA

Kwenye Ukingo wa Thim	-	Ebrahim Hussein
Morani	-	Emmanuel Mbogo
Kivuli Kinaishi	-	Said Mohamed
Nguzo Mama	-	Penina Muhando

5. Tathilitha, tarbia na sabilia ni miundo katika ushairi. Kwa kutumia mifano dhahiri, bainisha jinsi miundo hiyo ilivyotumiwa na washairi katika diwani mbili ulizosoma.
6. Kwa kutumia diwani mbili ulizosoma, eleza wajibu unaotakiwa kwa viongozi ili kukidhi vilio vyta watunzi wa mashairi. Toa hoja tatu kwa kila kitabu.
7. “Kuendelea kujadili nafasi ya mwanamke katika jamii ni upotevu wa rasilimali muda.” Tathmini kauli hiyo kwa kutoa hoja nne zenye mifano kwa kila kitabu katika riwaya mbili ulizosoma.
8. Bainisha vipengele vyta fasihi simulizi vilivyojitekeza katika tamthiliya mbili ulizosoma kwa kutoa hoja nne kila tamthiliya.